



Kevin Polston
Msimamizi wa Shule

Ofisi ya Msimamizi

Kentwood Public Schools
5820 Eastern Avenue, S.E.
Kentwood, MI 49508
Simu 616 • 455 • 4400

Agosti 4, 2021

Wapendwa Wazazi/Walezi na Wanafunzi:

Karibu katika mwaka wa shule 2021-22! Natumai mnafurahia msimu wa joto pamoja na wapendwa. Kwangu, Julai umekuwa mwezi wa furaha na bashasha, tangu nianze kutumikia kama msimamizi mpya wa Shule za Umma za Kentwood. Ni fahari kuu kushiriki katika kufungua ukurasa mpya katika Shule za Umma za Kentwood.

Asante kwa makaribisho kabambe niliyopokea katika jamii yote! Kuna fahari kubwa sana katika Kentwood na katika KPS. Natarajia kushirikiana na jamii yetu tunapojitahidi kuwa bora zaidi. Pamoja tunaweza kubadilisha ulimwengu kupitia kutoa fursa zinazofaa na zenye maana kwa wanafunzi wetu.

Katika shamrashamra za makaribisho, mnamo Julai 13, 2021, wanafunzi na wafanyakazi kutoka Shule za Umma za Kentwood walimkaribisha Gavana Gretchen Whitmer kwa Shule ya Upili ya East Kentwood kutia saina mswada wa kihistoria kuwa sheria ambayo hutoa rasilimali zaidi kwa wanafunzi wetu. Fedha hizi zitahakikisha kuwa kila mtoto anafikia mifumo ya msaada ambayo inaendelea kuimarisha ubora na usawa. Ningependa pia kuisitiza kwamba azimio letu, Ubora na Usawa katika Elimu, sio tu maneno matupu katika Shule za Umma za Kentwood. Ni ubora tunaoazimia kufikia kila siku kwa kila mwanafunzi.

Mwaka huu, tutasisitiza mada zifuatazo:

- **Afya na ustawi:** Tunapoendelea kupambana na janga hili la ulimwengu, lazima tuweke mbele afya za wanafunzi wetu, familia zao, na wafanyakazi wetu. Hakuna mtu anayepambana na janga peke yake; tutashinda pambano hili tukisimama pamoja kama jamii. Tafadhali tazama *Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara (F.A.Q.)* kwa maelezo zaidi juu ya mpango wetu wa usalama wa COVID. Usalama wa wanafunzi wetu, wafanyakazi, na jamii unabaki kuwa muhimu zaidi kwetu.
- **Kujitolea kwa kujifunza kuendelea na kuongozwa na data:** Tunataka wanafunzi washiriki kikamilifu katika kujifunza na kufaulu. Zaidi ya hayo, lazima tuige mfano huu kama shirika, kupitia ujifunzaji wa taasisi na kukusanya data ambayo inahakikisha tunatumia lugha moja ya nidhamu.
- **Ubora na Usawa:** Shule za Umma za Kentwood zimejitolea kwa ubora na usawa katika yote tunayofanya. Kuanzia ujenzi wetu wa dhamana hadi jinsi tunavyotumia dola za mlipa ushuru hadi jinsi tunavyomtendea kila mtoto wilayani, ubora na usawa ni “maadili tumizi” KPS.

Tunafurahi kuwakaribisha wanafunzi wetu kurudi katika masomo ya ana kwa ana! Mwaka uliopita tulikumbushwa juu ya umuhimu wa kuelimisha mtoto mzima na jukumu muhimu la mahusiano katika maisha ya watoto wetu. Mazingira ya masomo ya ana kwa ana na ushirikiano hutoka kwa wanafunzi wanaoshirikiana na walimu wao na wafanyakazi hutoa chaguo bora kwa wanafunzi wengi kufikia kiwango cha juu cha ujifunzaji.

SWAHILI

Utapokea taarifa kutoka kwa mkuu wa mtoto wako na tarehe muhimu za mwaka wa shule. Natarajia kuona wanafunzi wetu wote siku ya kwanza ya shule, Jumatatu, Agosti 23.

Kama ukumbusho, ikiwa bado hujakamilisha fomu ya uandikishaji mkondoni kwa wanafunzi wako, tafadhali fanya hivyo katika <https://www.kentwoodps.org/registration/olr/>

Kama kawaida, tafadhali usisite kuwasiliana na msimamizi wako wa jengo ikiwa una maswali maalum ya shule. Tafadhali usisite kuwasiliana nami na timu yetu ya ofisi kuu ikiwa una maswali ya wilaya. Tuko hapa kwa ajili yako na ya familia. Asante tena kwa msaada wako na usaidizi tunapoanza mwaka wa kusisimua mbele!

Wenu katika elimu,



Kevin Polston

Msimamizi